

2018

Matumizi ya neno “shikamoo” katika mtandao wa jamii forums: uchunguzi wa maana yake kimuktadha.

William, Daud

University of Dar es Salaam

William, D. (2018). Matumizi ya neno “shikamoo” katika mtandao wa jamii forums: uchunguzi wa maana yake kimuktadha. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

<http://41.86.178.5:8080/xmlui/handle/123456789/9615>

Downloaded from University of Dar es Salaam Library Repository

**Matumizi ya neno “shikamoo” katika mtandao wa jamii forums: uchunguzi wa maana
yake kimuktadha.**

Daud William.

Tasnifu ya MA Kiswahili

University of Dar es Salaam, Institute of Kiswahili Studies, 2018.

Utafiti huu unahusu maana ya neno “Shikamoo” kulingana na muktadha wa matumizi yake katika mtandao wa *JamiiForums*. Jumla ya majukwaa 12 ya mtandao huo yamehusishwa katika utafiti huu. Eneo letu la kiutafiti ni mtandao wa *JamiiForums*. Data ya utafiti huu imekusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni Maana kama Matumizi ya Ludwig Wittgenstein (1953). Mkabala wa kimaelezo ndio uliotumika katika uchambuzi wa data. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa kuna matumizi ya aina saba ya neno “Shikamoo” katika mtandao wa *JamiiForums* kutokana na jinsi lilivyotumiwa. Pia, imebainika kuwa neno “Shikamoo” limetumiwa katika miktadha nane ya kimatumizi. Kutokana na miktadha hiyo, neno “Shikamoo” limechanuza maana nane za kimuktadha. Kutokana na neno hilo kuchanuza maana nane tofautitofauti zinazotokana na muktadha wa kimatumizi, utafiti huu unapendekeza kuwa maana za neno hili pamoja na maneno mengine katika lugha, fasili zake katika kamusi zitolewe kwa kuzingatia miktadha ya kimatumizi. Kufanya hivyo, kutawasaidia wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili kung’amua maana na kutumia maneno kama hayo katika muktadha husika. Aidha, tafiti nyingine zinaweza kuchunguza miktadha ya matumizi ya maneno mengine kwa kuwa miktadha ni mingi na huendelea kuzaliwa kila siku kutokana na maendeleo ya jamii.